



**St. Walburg's Nyangao Referral Hospital**  
P. O. Box. 1002, Lindi Region - Tanzania, Mobile no. +255656227511  
Email address: [nyangaohospital@gmail.com](mailto:nyangaohospital@gmail.com) Website: <http://www.nyangaohospital.or.tz>

27/04/2026

## **TANGAZO LA KAZI**

Hospitali ya Rufaa ya Mt.Walburga Nyangao iliyoko Jimbo Katoliki la Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Mtama-Lindi inatangaza nafasi za kazi kama ifuatavyo;

### **1.0. Afisa Manunuzi na Ugavi II (Procurement and Supplies Officer) - Nafasi 1**

#### **1.1. SIFA**

- Wenye Shahada ya Ununuzi na Ugavi kutoka chuo kinachotambulika na serikali
- Kusajiliwa na Bodi kama 'Authorised Supplies Professional' na/au 'Certified Supplies Professional'
- Uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka 2

#### **1.2. Kazi na majukumu**

- Kuratibu na kushirikiana na idara za ndani ili kuelewa mahitaji ya manunuzi
- Kupitia na kuthibitisha maombi ya ununuzi (purchase requisitions) kwa usahihi na idhini stahiki
- Kufanya utafiti wa soko ili kubaini wasambazaji na fursa za upatikanaji wa bidhaa/huduma
- Kuitisha zabuni na kupata nukuu za bei zenye ushindani
- Kutathmini na kulinganisha nukuu za bei kutoka kwa wasambazaji kwa ajili ya kufanya maamuzi
- Kujadiliana na wasambazaji kuhusu bei, masharti ya usafirishaji, na vipimo/maelezo ya bidhaa
- Kushughulikia maagizo ya ununuzi (purchase orders), maombi ya ununuzi, na mabadiliko ya maagizo
- Kufuatilia na kuharakisha maagizo ili kuhakikisha yanawasilishwa kwa wakati
- Kuratibu upokeaji na ukaguzi wa bidhaa kwa kushirikiana na timu za ghala/logistics
- Kusimamia taratibu za kurejesha kwa wasambazaji bidhaa zisizokidhi viwango
- Kufuatilia utendaji wa wasambazaji katika ubora, gharama, na uwasilishaji kwa wakati
- Kuhakikisha uzingatiaji wa mahitaji ya maudhui ya ndani (Local Content Requirements) na kanuni za Tanzania
- Kuhifadhi kumbukumbu sahihi za manunuzi na nyaraka za ukaguzi
- Kusaidia udhibiti wa gharama kupitia ununuzi bora na majadiliano yenye tija
- Kuandaa na kuwasilisha ripoti za utendaji wa manunuzi
- Kudumisha viwango vya maadili katika manunuzi na uwazi
- Kusaidia maboresho endelevu ya mifumo ya manunuzi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**1.3. Mshahara:** Sawa na viwango vya mishahara ya serikali yaani TGS D

**2.0. Afisa Habari Msaidizi (Assistant Information Officer) - Nafasi 1**

**2.1. SIFA**

- Wenye Stashahada ya uandishi wa habari kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali

**2.2. Kazi na majukumu**

- Kupiga picha na kuandaa picha
- Kupiga na kuandaa picha mjongo (video clips)
- Kukusanya na kuandika habari
- Kuandaa majarida na mabango (posters) na vipeperushi
- Kukusanya takwimu mbalimbali
- Kuhifadhi picha na kuhudumia maktaba na marejeo
- **Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na mkuu wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake**

**2.3. Mshahara:** Sawa na viwango vya mishahara ya serikali yaani TGS C

**3.0. MASHARTI YA UJUMLA**

- Waombaji wawe ni raia wa Tanzania
- Wawe na umri wa miaka 25-40
- Waombaji waambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (Detailed CV) na picha ndogo za karibuni (passport size)
- Waombaji wenye uzoefu waonyeshe taarifa za taasisi walizofanyia kazi pamoja na waajiri wao
- Maombi yote yaambatanishwe na vyeti vya taaluma, vyeti vya sekondari na Baraza

**4.0. NAMNA YA KUOMBA**

Waombaji waandike maombi yao kupitia anwani ifuatayo;

MGANGA MFAWIDHI,  
HOSPITALI YA RUFAA YA MT. WALBURGA NYANGAO,  
S.L.P 1002,  
NYANGAO, LINDI.

Maombi yanaweza wasilishwa kwa mkono kwa kuleta moja kwa moja au kupitia barua pepe [nyangaohospital@gmail.com](mailto:nyangaohospital@gmail.com)

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **06/05/2026**

